



# **CHUO KIKUU CHA MACHAKOS**

**KUPASHA UMAHIRI KATIKA UFUNDI NA UTENDAJI WA  
BIASHARA**

## **UTENDAKAZI**

### **MAONO**

**Kuwa Taasisi ya kuigwa ya masomo ya juu**

### **AZIMIO**

**Kutoa nguvu-mali ya hadhi ya juu kupitia mafunzo mwafaka,  
utafiti, ushauri na huduma kwa jamii**

- k. Kutoa utaratibu, matokeo na huduma kwa njia inayolenga maadili ya utendaji haki kwa kila mtu.
- l. Kuwezesha uhamisho wa wanafunzi kati ya kozi mbalimbali zinazotolewa na taasisi mbalimbali za kimafunzo, vyuo vikuu na viwanda.
- m. Kukimu ustawi wa wafanyakazi na wanafunzi wote.

## **MAADILI**

Ili tuweze kutoa huduma nzuri kwa njia ifaayo tunaongozwa na maadili haya:

- Uadilifu - Kutimiza malengo yetu kwa washika dau wote
- Uaminifu - Kujenga imani kwa ushirikiano wa mawasiliano wazi
- Uwajibikaji - Kuwajibika katika utendaji wa kazi
- Utaaluma - Kutoa mafunzo ya juu tukizingatia mema kwa utendakazi wetu
- Ubunifu - Kujitolea kwa kuendelea kujiimarisha
- Usawa - Kuwa kielelezo kwa kujitolea kuwa chuo kinachoendeaza usawa katika utendakazi

## **WATEJA WETU**

Wafuatao ndio wateja wetu:

- Wakufunzi
- Wafanyakazi wa chuo kikuu cha Machakos
- Wanafunzi waliohitimu zamani na sasa
- Wazazi na walezi
- Wizara ya elimu ya juu, sayansi na tekinolojia
- Wizara zingine na idara za kiserikali
- Serikali za mitaa
- Jamii
- Taasisi za masomo ya juu
- Wafanyi biashara na wanakandarasi
- Mashirika yasiyo ya kiserikali na vikundi vya kijamii

- Mashirika ya kitaifa
- Viwanda
- Mashirika ya kidini

## **HUDUMA ZETU**

Huduma zetu kuu zinajumuisha mambo yafuatayo:

- Kutoa mafunzo ya kozi zote zinazotahiniwa
- Kushiriki katika shughuli za kijamii
- Kutoa huduma na vifaa vya malazi na mikutano
- Kutoa huduma za maandalizi na uchukuzi wa chakula nje na ndani ya chuo
- Kutoa huduma za urekebishaji na matengenezo
- Kufanya utafiti na ushauri katika nyanja za biashara, uongozi, utunzaji wa wateja na kadhalika
- Kutoa vifaa vya michezo na burudani
- Kutoa huduma za kuwashauri na kuwaelekeza wakufunzi, wafanyakazi na jamii kwa jumla

## **KIWANGO CHA HUDUMA ZETU**

Wateja wetu na washikadau yafaa watarajie kupata huduma za hali ya juu kama ifuatavyo:

- 1 Kutoa mafunzo ya:
  - Kozi za shahada kama inavyohitajika
  - Stashahada kwa kati ya miaka miwili na mitatu na kutahiniwa na baraza la mitihani nchini Kenya (KNEC) na chuo kikuu cha Kenyatta
  - Kozi ya kiufundi kwa miaka miwili na kutahiniwa na baraza la mitihani nchini Kenya (KNEC) na chuo kikuu cha Kenyatta.
  - Kozi za hatua kwa hatua za astashahada na stashahada za miezi sita kwa kila hatua na kutahiniwa na baraza la mitihani nchini Kenya (KNEC) na chuo kikuu cha Kenyatta
  - ATC/CPA/CPS kwa miezi sita kwa kila hatua na kutahiniwa na KASNEB

- 2 Kushughulikia maswala ya wageni kwa njia ya heshima na kwa wakati ufaao.
- 3 Kujibu maswali yote katika muda usiozidi siku tano.
- 4 Kushughulikia malalamishi ya wanafunzi papo hapo.
- 5 Kutatua kesi za wanafunzi za utovu wa nidhamu katika muda wa majuma mawili.
- 6 Kutoa notisi ya siku kumi na nne ya mikutano kwa wateja wetu na washikadau
- 7 Kutayarisha malipo kwa bidhaa na huduma katika muda wa mwezi mmoja baada ya kupokea stakabadhi husika kulingana na sheria ya ununuizi.
- 8 Kutayarisha vitabu vya hesabu kwa lengo la ukaguzi kufikia tarehe mosi Agosti kila mwaka.
- 9 Kufanya urekebishaji wa dharura mara moja na urekebishaji mwingine kulingana na ratiba.
- 10 Kukamilisha mipango yote kulingana na muda wa kandarasi.
- 11 Kutoa malipo kwa asasi zote kwa muda uliowekwa.

## **HAKI ZA WATEJA WETU**

Wateja wetu wana haki zifuatazo:

- Kupewa majibu ya maswali yao bila kutozwa malipo.
- Habari na harifa zao kushughulikiwa kwa siri.
- Kufikia habari inayohitajika pamoja na majibu ya utekelezaji wa maazimio.
- Kupewa majibu kuhusu maswali, malalamishi na maombi yao kwa heshima na wakati ufaao.
- Kupata malipo ya huduma na bidhaa zilizopokelewa kulingana na maafikiano na kupata stakabadhi zote husika.
- Kupata mafunzo ya kitaaluma kulingana na silabasi iliyoidhinishwa
- Kupata mazingira mazuri kiusalama na kiafya
- Kutumia vifaa na huduma ya taasisi bila kuhangaishwa na yejote.
- Kupata risiti kwa malipo yoyote.

## **MAJUKUMU YA WATEJA WETU**

Wateja wetu wana majukumu yafuatayo:

- Kujifahamisha na kufuata amri za chuo
- Kutoa habari muhimu zinayohitajika bila kusita ili kutuwezesha kutoa majibu kwa wakati ufaao.
- Kutupatia uhakiki unaotujenga
- Kuwaonyesha heshima wafanyikazi wetu
- Kulipia huduma na bidhaa wanazopewa
- Kuzingatia urasmi na uadilifu katika maingiliano yao nasi.
- Kutoa maoni yao kuhusu jinsi wanavyoziona huduma zetu.
- Kuhakikisha kuwa kuna risiti kwa malipo yoyote.
- Kuwa na uwazi na uaminifu
- Kutoa huduma na bidhaa (haswa wafanyabiashara na wanakandarasi) kulingana na maelezo yetu.

## **MAFUNZO**

Tunatoa mafunzo katika kozi zifuatazo:-

### **A. KOZI ZA SHAHADA**

1. Shahada ya sayansi katika kompyuta/tarakilishi
2. Shahada ya sayansi katika ufundu wa nguvu/vifaa vya umeme
3. Shahada ya sayansi katika ukarimu na utalii
4. Shahada ya ubadilishanaji na ugawaji wa bidhaa.
5. Shahada ya elimu katika masomo ya hesabu na biashara
6. Shahada ya elimu katika masomo ya hesabu na fizikia
7. Shahada ya elimu katika sayansi kimu

### **B. KOZI ZA STASHAHADA**

1. Uhandisi wa magari
2. Teknolojia ya ujenzi

3. Technolojia ya mavazi
4. Uhandasi wa elektroniki
5. Usimamizi wa mashirika
6. Utaalamu wa vyakula na upishi
7. Uhandisi wa nguvu za umeme
8. Uhandisi wa umekaniki (uzalishaji)
9. Tekinolojia ya mawasiliano (kwa viwango)
10. Usimamizi wa biashara
11. Usimamizi wa wafanyikazi (kwa viwango)
12. Ununuzi na uthibiti wa bidhaa
13. Mafunzo ua uhazili
14. Utaalamu wa ugavi/ugawaji
15. Uhasibu
16. Uhandisi wa miundo misingi
17. Usanifu majengo
18. Uhandisi wa umekaniki (Ukarabati wa vifaa na mitambo)

#### C. KOZI ZA ASTASHAHADA

1. Ufundi wa magari
2. Ufundi wa nguvu za umeme
3. Ufundi wa vifaa vyaa umeme
4. Ufundi wa kuchomelea
5. Uhandisi wa mekaniki
6. Ujenzi
7. Ufundi wa mbao
8. Utaalamu wa vyakula na upishi
9. Ufundi wa nguo
10. Mafunzo ya uhazili
11. Ununuzi na uthibiti wa bidhaa
12. Usimamizi wa biashara
13. Usimamizi wa wafanyikazi

#### **D. KOZI ZA KASNEB**

1. Uhasibu (1 – 6)
2. Astashahada ya uhasibu
3. Tekinolojia ya mawasiliano (CICT)

#### **E. KOZI NYINGINE**

Kozi za DIT:-

1. Ufundi wa magari
2. Utaalamu wa ulaiki
3. Ufundi wa kuchomelea
4. Ujenzi
5. Ufundi wa mbao
6. Ufundi wa nguo
7. Ufundi wa kuunganisha nyaya za stima
8. Kuchomelea kwa gesi
9. Ufundi bomba
10. Usanifu majengo

#### **HUDUMA YA UELEKEZI/USHAURI**

- Kushughulikia wateja
- Mahusiano ya umma
- Stadi za uongozi
- Ushauri/Mawaidha
- Uuzaji
- Mawasiliano
- Maswala ya pesa na ushuru
- Uhandisi
- Utafiti
- Ufundi wa magari
- Maswala ya mipango na utendakazi

## **KUHAKIKIWA KWA NAKALA YA UTENDAKAZI**

Nakala ya utendakazi itahakikiwa kulingana na mahitaji ya chuo

### **MAONI**

- Malalamishi, shukrani na mapendekezo yapelekwe kwa wakuu wa idara na iwapo mteja haridhiki, yapelekwe kwa mwandamizi wa chuo.
- Maoni yaweza pia kuwasilishwa kupitia simu, barua pepe na visanduku vyatmaoni
- Tutaheshimu siri zote
- Maoni yote yatashughulikiwa kabla ya siku saba.

### **MPATANISHI**

Mkuu wa chuo

Chuo Kikuu Cha Machakos

S.L.P. 136-90100

### **MACHAKOS**

|                      |  |
|----------------------|--|
| Nambari ya simu      | 044-21604  |
| Kipepesi             | 044-20353  |
| Simu ya mkono/Rununu | +254 735 – 247939<br>+254 723 – 805829   |
| Barua pepe           | <a href="mailto:info@machakosuniversity.ac.ke">info@machakosuniversity.ac.ke</a> |
| Anwani ya tovuti     | <a href="http://www.machakosuniversity.ac.ke">www.machakosuniversity.ac.ke</a>   |



# **CHUO KIKUU CHA MACHAKOS**

## **UTENDAKAZI KWA WANANCHI**

| Huduna Inayopeanwa                 | Hitaji                            | Malipo ya wateja                     | Muda                                 |
|------------------------------------|-----------------------------------|--------------------------------------|--------------------------------------|
| Ufundi                             | Kulingana na baraza la mitihani   | Mwongozo wa malipo ya karo           | Kulingana na mahitaji ya kozi husika |
| Majibu                             | Bila                              | Bila Malipo                          | Siku mbili                           |
| Malalamishi ya wateja              | Bila                              | Bila malipo                          | Kwa siku tano                        |
| Notisi ya mikutano                 | Kulingana na hitaji               | Bila malipo                          | Wiki mbili                           |
| Kutoa malipo                       | Stakabadhi ya malipo              | Bila malipo                          | Siku tisini                          |
| Kutayarisha vitabu vya hesabu      | Sera ya serikali                  | Bila malipo                          | Agosti mosi, kila mwaka              |
| Malipo kwa asasi zote              | Sera ya serikali                  | Bila malipo                          | Kulingana na hitaji                  |
| Kuingia                            | Ustahilifu wa kozi                | Astashahada - 500/= Shahada - 1000/= | Kulingana na ratiba ya kuingia       |
| Kubadili kitambulisho kilichopotea | Kuripoti kupotea                  | Shilingi mia mbili                   | Wiki moja                            |
| Kutoa chapa (Uchapishaji)          | Idhini ya uchapishaji             | Bila malipo                          | Papo hapo                            |
| Kutoa chapa (Uchapishaji)          | Kutokuwa na idhini ya uchapishaji | Shilingi mbili                       | Papo hapo                            |